



Bw. Marshall D. Orson, Mwenyekiti Bodi
 Bi. Vickie B. Turner, Mwenyekiti Msaidizi
 Bw. Stan O. Jester
 Dkt. Michael A. Erwin
 Bi. Allyson Gevertz
 Bw. Dijon DaCosta
 Dkt. Joyce Morley

Bi. Cheryl Watson-Harris, Msimamizi wa Muda

INAPASWA KUCHAPISHWA BILA KUKAWIA

Sept. 15, 2020

Mawasiliano:

Portia Kirkland, 678-427-4898
 Carla Parker, 404-734-1717

Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb Yatangaza Mpango wa Kufungua Tena

STONE MOUNTAIN, Ga. – Msimamizi wa Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb, Cheryl Watson-Harris na timu yake wamewasilisha mpango uliosashwa wa kufungua tena wa Wilaya katika mkutano wa Bodi ya Elimu wa Sept. 14. Maamuzi yamefikiriwa kwa umakini kwa kuzingatia hali ya COVID-19 na shule kufungwa tangu Machi 16, 2020.

Hapo awali Wilaya ilichelewesha kuanzisha mwaka wa masomo wa 2020-21 na ikafungua shule na mfumo wa kusoma mtandaoni ili kupunguza COVID-19 kuenea katika jamii. Mpango wa sasa wa kufungua tena unataka mfumo wa masomo ulingane na mpango husika wa kudhibiti kuenea kwa magonjwa katika jamii. Ikiwa magonjwa yanaenea kidogo au hata hayaenei, basi mfumo wa kawaida utatumika. Ikiwa magonjwa yanaenea kidogo au kwa wastani, aidha mfumo wa masomo ya kawaida, mseto au ya mtandaoni yatatumika.

Kulingana na data ya Sept. 14 2020, kiwango cha hatari cha kuenea kinasalia juu katika Kaunti ya DeKalb. Kwa sasa, kuna zaidi ya visa 100 kwa wakazi 100,000 kwa kipindi cha siku 14. Mpango wa awamu wa Wilaya ni wa kihafidhina na wa polepole kwa sababu usalama na maslahi ya wanafunzi na wafanyakazi ndio unasalia kipaumbele. DCSD itaenda kwa awamu ya mbili ya mpango wake wa kufungua tena wakati kuna visa 100 au chini kwa wakazi 100,000 katika kipindi cha siku 14.

Katika awamu ya pili, wanafunzi watasalia katika masomo ya mtandaoni. Pia katika awamu ya pili, wafanyakazi wa DSCD watahamia kwa mazingira mseto ya kufanya kazi, kwa hivyo kufanya kazi katika majengo kwa siku mbili kwa wiki na kwa mbali kwa siku tatu. Kabla ya mpito huu wa awamu ya tatu, wanafunzi wa gredi ya pili, sita na ya tisa watakuwa n siku moja ya masomo ya ana kwa ana. Hii itawawezesha wafanyakazi wa shule kuwa na kipindi cha kuzoea kabla ya kutekeleza awamu ya tatu kikamilifu na wanafunzi wote. Ufuatiliaji wa karibu wa data ya COVID-19 utabainisha wakati DCSD itahamia polepole kwa awamu ya nne na ya tano.

Wilaya itatekeleza mbinu ya “awamu” ili kuruhusu shughuli za wanariadha na za baada ya masomo kurejea. Kushiriki ni kwa hiari. Hakuna jukumu la wanafunzi, makocha, au wafadhili kushiriki. Shule zitaendelea kupunguza hatari ya kuambukizwa kwa kudumisha umbali kati ya watu wakati wa mazoezi na wakati wanafunzi hawamo uwanjani wakicheza. Barakoa/vifunika uso vinahitajika.

“Usalama na ustawi wa wanafunzi wetu ndio kipaumbele cha Wilaya. Mipango yote inategemea kuwa na chini ya visa 100 kwa watu 100,000. Data hii ni ya kutazamia hatari ya kuwa katika eneo salama. Wazazi watakuwa na chaguo la kuendelea na masomo ya mtandaoni, na wilaya itaendelea kuwasiliana na familia tunapokuwa tukihamia awamu hizi,” Msimamizi Watson-Harris alishiriki na bodi.

Mpango wa Wilaya umejumuisha mwongozo wa sasa kutoka kwa Idara ya Afya ya Umma ya Georgia, Halmshauri ya Afya ya Kaunti ya DeKalb, Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDS), Idara ya Elimu ya Georgia (GaDOE), Shirika la Huduma ya Elimu Mjini (MRESA) kwa kushirikiana na wasimamizi, na maafisa wa ndani na wa serikali.

Utafiti wa pili umezinduliwa ili kupokea maoni ya washikadau kuhusu uwezekano wa kufungua tena. Makundi mahsusni yatakutanika na wasimamizi, waalimu na washikadau wengine. Mpango huu unaweza kubadilika na unategemea data na maoni ya washikadau.

Wilaya itaendelea kufuatilia data ya COVID-19 na kutathmini kiwango cha kuenea ili kubainisha ni lini mfumo wa sasa wa masomo unapaswa kurekebisha. Tathmini inayofuata itawasilishwa wakati wa mikutano ya bodi mnamo Okt. 19, Nov. 9 na Des. 7, 2020.

Bofya hapa ili kupitia uwasilishaji wote, ikiwemo maelezo kuhusu itifaki zilizosasishwa za usafishaji na matengenezo.